Ujio Wa Ukristo
(The Triumphs Of Christianity)

na

Ellis P. Forsman

Ujio Wa Ukristo
(The Triumphs Of Christianity)

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Ujio Wa Ukristo

2 Kor. 2:14

2 Kor. 2:14, "*Ila Mungu ashukuriwe, anayetushangiliza daima katika Kristo, na kuidhihirisha harufu ya kumjua yeye kila mahali kwa kazi yetu.*"

Katika kucheza, kazi, au vita tunapenda kuwa katika upande unaoshinda; hakuna anayejali kukubaali kuwa ameshindwa.

Nyaraka zilizoandikwa na Paulo Mtume aliyevuviwa zimejawa roho za ujio.

Katika kifungu kuna mpasuko wa shukurani toka kwa mtume.

Yawezekana Pauli alifikiria kuingia kwa ujio wa jenerali wa Kirumi, ambaye baada ya ushindi wa baadhi ya kampeni, alirudi katika mji mkuu wa Rumi, aakiwa na majipu ya vita ili apokee heshima ya vita.

Ndivyo ilivyo kwa Mkristo. Maisha yake yamejawa na vita na miangaiko, lakini taji ya uzima imeahidiwa kwa wale watavumilia kwa imani hadi mwisho.

Ujio Wa Kanisa

Juu ya Uyahudi.

Kanisa lilizaliwa na adui huyu.

Mafarisayo walimjeruhi Yesu hadi kifo cha msalaba kwa sababu aliukataa unafiki wao.

Lakini kwa uchache unaotisha upofu wa kitisho cha Kalvari uliingia katika moyo wa kiongozi wa Kiyahudi, pale ilipoibuliwa tena na matukio ya Pentekoste wakati Wayahudi 3000 walipozidishwa katika kanisa.

Juu ya Filosofia ya Kigiriki.

Hii haikuwa kwa mudaa mrefu na uchungu wa vita dhidi ya Uyahudi.

Paulo aliungilia kati katika Areopago.

Mdo. 17:22-31, "*Paulo alisimama katikati ya Areopago akasema enyi watu wa Athene, katika mambo yote naona ya kuwa ninyi ni watu wa kutafakari sana mambo ya dini. Kwa sababu nilipokuwa nikipita huko na huko na kuyaona mambo ya ibada yenu, naliona madhabahu iliyoandikwa maneno haya, KWA MUNGU ALIEYEJULIKANA. Basi mimi nawahubirini habari zake yeye ambaye ninyi mnamwabudu bila kumjua. Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye kwa kuwa ni*

Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono; wala hatumikiwi kwa mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji kitu chochote; kwa maana ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vutu vyote. Naye alifaanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani, na mipaka ya makazi yao; ili wamtafute Mungu ingawa ni kwa kupapasa papasa, wakamwone, ijaapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu. Kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda na kuwa na uhai wetu. Kama vile mmoja wenu mtunga mashairi alivyosema, maana sisi sote tu wazao wake. Basi kwa kuwa sisi tu wazao wa Mungu, haitupasi kudhani ya kuwa Uungu ni mfano wa dhahabu au fedha au jiwe, vitu vilivyochongwa kwa ustadi na akili za wanadamu. Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu. Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu."

Juu ya mateso ya Kipagani.

Ilionekana haiepukiki kwamba kuenezwa kwa injili ingeweza kuileta kaika mvutano na ufalme wa Kirumi, na huu mvutano ulikuwa wa muda mrefu na mchungu.

Kulingana na Foxes Book of Martyrs, kutoka 67 A.D. hadi 323 A.D. Rumi ililkuwa ikiongozwa na wakuu kumi watata, ambayo ilimanisha miongo kumi ya mateso dhidi ya kanisa.

Chini ya msaada wa Mungu, hataivyo, kanisa lilikutana na machafuko haya na ikaingia juu yake.

Kanisa linakumbana na pingamizi kama hayo leo

Ukifanana na machafuko dhidi ya Uyahudi, kanisa leo linaingia kwenye machafuko na ulimwengu wa madhehebu.

Kuhubiriwa kwa injili sio <u>tu</u> njia, bali <u>ni</u> njia ya wokovu.

- Mdo. 16:17, "*Akamfuata Paulo na sisi akipiga kelele, akisema, watu hawa ni watumishi wa Mungu aliye juu, wenyewe kuwahubiria njia ya wokovu.*"
- Yohana 14:6, "*Yesu akamwambia, mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi.*"

Hii kiualisia inangiza kutokuwa na furaha kwa wale wanaoshikilia kwamba kuna njia nyingi za kuweza kuokolewa.

Biblia inafundisha kwamba kuna njia moja pekee ya kuwa Mkristo

- Mdo. 2:36-38, "*Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulubisha kuwa Bwana na Kristo. Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, tutendeje ndugu zetu? Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"
- Mdo. 2:41, "*Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.*"
- Mdo. 2:47, "*Wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.*"

Kiualisia, hii inaibua mapingaamizi kwa wale wanaoshindania njia zingine za maongezi.

Biblia inatupatia jina la kidini la "Mkristo" kwa watu wa Mungu ili waweze kulivaa kwa heshima ya Kristo Mwokozi wetu.

- Mdo. 11:26, "*Hata alipokwisha kumwona akamleta Antiokia. Ingawa kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika pamoja na kanisa na kuwafundisha watu wengi. Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia.*"
- Mdo. 26:28, "*Agripa akamwambia Paulo, kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo.*"
- 1 Pet. 4:16, "*Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya, bali amtukuze Mungu katika jina hilo.*"

Mashindano ya kutumia jina la Kristo katika kuondoa majina yote ya wanadamu yakiingizwa katika ukengeufu wa wale wanaoshindana katika kuvaa majina ya wanadamu.

- Mdo. 4:10, "*Jueni ninyi nyote na watu wote wa Israeli ya kuwa kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye ninyi mlimsulubisha, na*

Mungu akamfufua kaatika wafu, kwa jina hilo mtu huyu anasimama ali mzima mbele yenu."

- Mdo. 4:11-12, "*Yeye ndiye jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi, nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la pembeni. Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.*"

Biblia inafundisha kwamba Wakristo wanapaswa kuungana katika mwili mmoja.

- Yohana 17:20-21, "*Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja kama wewe Baba ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.*"

- 1 Kor. 1:10, "*Basi ndugu nawasihi kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja.*"

- Efe. 4:4-6, "*Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, imani moja, ubaatizo mmoja. Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote.*"

Kilio hiki cha umoja wa Wakristo katika mwili mmoja kiualisia unamanisha kukataa udhehebu, ambayo, kimsingi, inaleta ghadhabu ya ulimwengu wa madhehebu.

Sawa na machafuko dhidi ya Wanafilosofia wa Kiyunani, kanisa leo iko katika machafuko na wanatheolojia wa kisasa wanaojiita Wakisasa.

Agano Jipya linafundisha kwamba Yesu alizaliwa na bikira; akafanya miujiza baada ya miujiza wakati wa huduma yake duniani; akafa kifo cha kutisha msalabani kwa ajili ya dhambi ya ulimwengu; alizikwa, lakini aakafufuka kutoka katika wafu; na baada ya kupaa kwenda mbinguni, alituma Roho Mtakatifu kwa mitume ili awaongoze katika kweli yote.

Yote haya yanakataliwa na wale walio na nguvu katika ukisasa, na kiualisia wale wanaoshindania uasili huu ukweli utashinda wale wa kisasa wanaopinga.

Ujio wa injili ya Kristo

Uliwapa Wakristo ushindi dhidi ya dhambi

Juu ya hatia ya dhambi.

Rum. 3:23, "*Kwa sababu wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.*"

Uyahudi usingeondoa dhambi.

Heb. 10:4, "*Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi.*"

Ilikuwa ni mpango wa Mungu kwamba kupitia kifo cha Kristo, ukombozi wa mwanadamu kutoka dhambini ukamilishwe.

1 Pet. 1:18-19, "*Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha aau dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani ya Kristo.*"

Juu ya nguvu ya dhambi – juu ya majaribu.

- 1 Kor. 10:13, "*Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili.*"
- 2 Pet. 2:9, "*Basi Bwana ajua kuwaokoa watauwa na majaribu, na kuwaweka wasio haki katika hali ya adhabu hata siku ya hukumu;*"

Iliwapa Wakristo ushindi juu ya majaribu ya maisha.

Juu ya huzuni.

2 Kor. 1:3-5, "*Na ahimidiwe Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema, Mungu wa faraja yote; atufarijiye katika dhiki zetu zote ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizzo tunazofarijiwa na Mungu. Kwa kuwa kama vile mateso ya Kristo yanavyozidi kwetu, vivyo hivyo faraja yetu inazidi kwa njia ya Kristo.*"

Juu ya magumu.

Ayubu 14:1, "*Mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke siku zake za kuishi si nyingi, naye hujaa taabu.*"

Ugumu, marabara za miinuko inaweza kuinuka mbele yako, lakini Yesu ambaye hana ukomo katika nguvu na upendo ameahidi uwepo wake na msaada kila wakati wa hitaji.

- Mat. 28:20, "*Na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari.*"
- Heb. 13:5, "*Msiwe na tabia ya kupenda fedha; mwe radhi na vitu mlivyo navyo; kwa kuwa yeye mwenyewe amesema, sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa.*"
- Zab. 50:15, "*Ukaniite siku ya mateso; nitakuokoa, na wewe utanitukuza.*"

Juu ya uoga.

- Zab. 27:1, "*BWANA ni nuru yaangu na wokovu wangu, nimwogope nani? BWANA ni ngome ya uzima wangu, nimhofu nani?*"
- Zab. 46:1, "*Mungu kwetu ni kimbilio na nguvu, msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso."*
- Heb. 13:5-6, "*Msiwe na tabia ya kupenda fedha; mwe radhi na vitu mlivyo navyo; kwa kuwa yeye mwenyewe amesema, sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa. Hata twathubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa; mwanadamu atanitenda nini?*"

Juu ya dunia.

1 Yohana 5:4, "*Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu.*"

Iliwapa Wakristo ushindi juu ya kifo chenyewe.

- 1 Kor. 15:20-22, "*Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala. Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhalika na kiyama ya wafu ililetwa na mtu. Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa.*"
- 1 Kor. 15:55-57, "*Ku wapi, ewe mauti, kushinda kwako? U wapi, ewe mauti uchungu wako? Uchungu wa mauti ni dhambi, na nguvu ya dhambi ni torati. Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.*"
- 1 Thes. 4:13-17, "*Lakini ndugu hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini.*

Maana ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka vivyo hivyo na hao walio lala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakao salia hata wakati wa kuja kwake Bwana, haakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele."

Hitimisho

Hakika, Mkristo mara zote anaweza kusema:

2 Kor. 2:14, "*Ila Mungu ashukuriwe, anayetushangiliza daima katika Kristo, na kuidhihirisha harufu ya kumjua yeye kila mahali kwa kazi yetu.*"

Kumbuka kwamba ujio huu ni katika uzima, katika mauti, na katika umilele ni katika Kristo Yesu.

Je uko katika Kristo? Kama siyo, njoo upande wa Bwana; upande wa ushindi, upande wa wokovu.

Haya ndiyo unaweza kufanya ili hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb. 11:6, *"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao."* Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na mimi akniambia kwamba haamini kwamba Mungu yuko. Kwa vile nilisha batizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu mandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba Mungu yuko. Lakini ili kuwa upande salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani atampeleka mbinguni (kama kuna mbingu), na si motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matend. 2:38, *"Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* Matend

11:18, *"...Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima."* Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "Kwamba kuna mwizi!" taratibu unachukua simu ya mkononi, unawapigia polisi. Kidogo polisi wanafika na kumshika mwizi. Alafu anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Toba iliyokweli ni kwamba mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena.

Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Tunatakiwa kufanya hivyo kabla hatujawa wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, *"Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."*

Tuna kiri nini? Kwamba tuna amini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.
Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekeza kwenye kitu Fulani; si kwamba mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kuitimiza haki yote, *"Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni mwanangu mpendwa, ninaye pendezwa naye."* (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo sahihi la kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*Imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote."* Tuna batizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, si kwa sababu ni haki yetu.

Kwa kweli, tusipo batizwa, tungali katika dhambi zetu. *"Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matend. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "*Kwa ajili ya ondoleo la dhambi*". Kwa nini watu wanapenda kuach hatua inayotuondoa dhambi zetu?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. *"Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu iki hiki, "*Unakawilia nini? Simama, na ubatizwe, na uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko, *"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale umekufa. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlvyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika katika mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusiitumikie dhambi tena."* (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumiwa na damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru na dhambi zetu za zamani kama tu tukibatizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuwezi kupeleka maiti makaburini, na kumwekea udongo kidogo juu yake; tunauzika mwili.

Kama hujafanyika Mkristo, kwa nini usifanyike leo?